

Shairi lifuatalo liliandikwa na Hassan Adam kwa ajili ya kulijibu shairi la Yusuf Kalala wa Washington DC, kuhusiana na shairi lake la pendo hili pendo gani, kwangu lanitakani?

MPENDE AKUPENDAE

- | | |
|--|---|
| <p>1. Pendo lisikusakame, kupenda kwetu wajibu.
Kwingine usitazame, mpende huyo habibu.
Mwili usikuzizime, kama yeye haghilibu.
Mpende akupendae, sipende asokupenda!</p> <p>2. Pili hapa nabashiri, wengi wao ni madubu.
Wajifanyao wazuri, kumbe yao kuharibu.
Kwa mini zao hariri, zilowakumba swahibu.
Mpende akupendae, sipende asokupenda!</p> | <p>3. Beti tatu ni shairi, fupi yangu ni majibu.
Zingatia ushauri, ujue wako wajibu.
Isikumeze bahari, ukaacha ya wajibu.
Mpende akupendae, sipende asokupenda.</p> <p style="text-align: right;"><i>Hassan Adam (HAU)
Cologne, Ujerumani.
August, 2002</i></p> |
|--|---|